# MWILI WA MBINGUNI, ULIO WA KIROHO UNATUNGOJEA SISI

*Yohana Mt: 1:1-5: Hapo mwanzo kulikuwako Neno (Logos), naye Neno alikuwako kwa Mungu, Naye Neno alikuwa Mungu. Huyo mwanzo alikuwako kwa Mungu. Vyote vilifanyika kwa huyo; wala pasipo yeye hakukufanyika chochote kilichofanyika. Ndani yake ndimo ulimokuwa uzima, na ule uzima ulikuwa Nuru ya watu nayo Nuru yang'aa gizani wala giza halikuiweza.*
*Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa Neema na kweli.*

Hebu tusikilize kile Nabii wa Mungu wa siku zetu alichokisema juu ya hilo:

Hebu tufunge macho yetu kwa mawazo yetu kwa dakika chache/muda kidogo na twende mbali kidogo kabla hakujawa na chochote. Ile chemchem kuu ya milele yote ilikuwa ile Roho ya upendo, Furaha; ile Roho ya uadilifu, ile Roho ya ukweli katika huu ukamilifu. Na katika kuishi kwa baba alitokea yule Logos ambaye alikuwa ni Mwana, ambaye ni yule (theophany) mwili unaonekana, ambao ulikuwa ni mwili wa yule Jehovah mkuu Mungu aliyeishi katika mwili huu wa kimbinguni. Ambaye ndiye yule Logosi. Lile Neno lililonenwa kutoka kwa zile chemichemi kuu za uzima na zikaendelea. Na pale palikuwa na ule mwili unaonekana wa Mungu (theophany). Ambao ulikuwa ni Mungu akifanyika kuwa Neno.

Halafu sasa ile theophary (mwili wa neno) ulifanyika mwili katika utu wa Kristo Yesu (2 Kor 5:17-19). Na ukamilifu wote wa utatu ulikaa ndani yake, vyote Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, vyote katika huyo (Wakolosai 2;9-10). Na hiyo ndiyo njia tuiendayo kurudi kule nyuma kwenye mwanzo asilia ya Mungu hapo tumezaliwa upya sio kwa mwili, Tumezaliwa tena siyo kwa damu, lakini wamezaliwa tena kwa Roho (1Petro 1:22-23) Na katika yule Roho wa milele wa upendo na uadilifu anashuka chini kuja kukaa ndani yetu.

Na hapo sasa tunapokufa kutoka maisha haya, tunaenda kwenye mwili ……kama maskani yetu iliyo ya dunia ikiharibiwa, tunao (theophany) mwili wa kimalaika tunaoingia ndani yake, mwili wa kimbinguni
2Kor 5:1-9

Halafu wakati wa kuja Bwana Yesu, huu mwili unachukuliwa tena kutoka ardhini tena na kuumbwa katika hali ya utukufu kuishi katika uwepo wake milele



(Wathesalonike 4:16-17). Halafu sasa upotofu wote, mambo yote ambayo yalikuwa kwenye upotovu yote yanakoma na kufutika. Mwili unaenda kwenye adhabu yake. Kuzimu kunafumbua kinywa chake na kuumeza uovu wote na upotofu. Na Mungu na kanisa lake, mpendwa, Bibi Arusi wake, wanachukuwa nafasi zao kwa milele yote na kuendelea. Hilo ndilo tumaini kuu la kanisa la kikristo.

Halafu nilikuwa ninafikiria usiku wa jana baada ya kurudi nyumbani, nikiwa nimelala kwa dakika chache, Nilikuwa ninafikiria inavyokuwa baada ya nafsi kuondoka ndani ya mtu ni nini hasa?. Ni utu wake wa ndani umemtoka (2Kor 4:16). Yeye hajakufa; bado anaishi unaona, anaishi milele. Na wapendwa wetu waliotangulia kupita nje ya pazia hili wanaishi katika miili ambayo hatujui ikoje (Yohana Mt 14:1-3) bado haijafunuliwa.

Kuna hatua tatu za kila kitu. Kuna hatua ya mwili huu unaokufa (I Kor 15:53), kuna mwili ule usiokufa na halafu mwili wa utukufu (mwili wa ufufuo) kama vile tu, vitu vingine, kama Baba, Mwana na Roho Mtakatifu vinaenda mahali pamoja, na hawa watatu wanamfanya huyu mmoja kuhesabiwa haki kwa Imani, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu katika njia hiyo humfanya huyommoja. Na nafsi, mwili, na roho vinamfanya mmoja. Na inasafiri katika hali tatu, na hawa watatu ni mmoja.

Na wakati nafsi inapouacha mwili, inachukuwa safari yake mpaka mahali pa mapumziko katika mwili ambao uko kwa namna na umbile la mwili huu, lakini sio kama mwili huu. Lakini mwili ule ulio namna ya kama mwili wa kimbinguni, inaporudi tena duniani, inachukua chembechembe ambazo iliishi ndani yake na hapo inakuwa mwili uliotukuzwa (Matayo 27:51-53). Huo mwili ndio ambao tutamuona Bwana Yesu katika huo wakati wa ufufuko wa mwili (I Kor 15:42-44,48-49.

"Wala haijadhihirika bado tutakavyokuwa: alisema Yohana. Lakini twajua yakuwa (tutafanana naye) tutakuwa na mwili kama mwili wake wa utukufu kwa maana tutamuona kama alivyo" (1Yoh 3:2) na mikono hii yote ya kizee iliyo na mikunjokunjo na nyama zilizo sugu, vyote vitatoweka na kujiwa na uzuri wa ujana. Ninyi wanaume na wanawake wazee, kumbukeni huo uzee wenu ni alama ya anguko, (Rumi 8:19-23, 2 Kor 5:2-4). Lakini katika ufufuo hakutakuwa na alama yoyote ya dhambi. Lakini kwa nini Mungu alikufanya kama alivyokufanya? Akakuleta wewe katika umri fulani wakati ulipokuwa na miaka ishirini na mbili, miaka ishirini na tatu, ulikuwa katika kiwango chako cha ubora. Ulikuwa unakula chakula na unazidi kupata nguvu na afya, na ulionekana mtu mwenye nguvu. Halafu baada ya hapo ukaanza kuwa na makunyanzi unaona, kifo kimeshaanza. Lakini katika ufufuo namna zote za uzee zitafutiliwa mbali.

Mtoto anapoumbika (mimbani) katika tumbo la mama, anao uhai wa aina fulani moja. Lakini kwanza ni Roho, na kadiri ile Roho (uhai) unapoanza kuchukua mwili, ile chembe ndogo ya uzima inaanza kuchukua mwili, na mara tu anapotoka katika……..sasa, katika tumbo ni misuli inayocheza, ni midogo ikitetemeka. Tunajua hilo. Hizo ni chembe chembe ndogo.

Lakini mara tu anapozaliwa katika hii dunia na anavuta pumzi yake ya kwanza, anakuwa nafsi iliyo hai unaona? Mara tu ule mwili unapozaliwa katika dunia, uko mwili wa mbinguni, au mwili wa kiroho, kuungana na huo. Na mara tu huu mwili wa asili unapozaliwa, uko mwili wa kimbinguni unaosubiri huo kama maskani yetu ikiharibika, yako maskani ya kimbinguni yanayotungojea" (2Kor 5:1) Mara tu ule mwili unapozaliwa hapa duniani, uko mwili wa kiroho unangojea kuupokea huo. Na mara tu ule mwili wa asili unapoharibika, uko mwili wa kimbinguni unaongojea kule ng'ambo, mwili wa kimalaika tunauita (theophany) mwili wa kimalaika.

Mara tu tunapotoka kwenye mwili huu, tunaingia ndani ya mwingine mmoja usiohitaji maji baridi, hauhitaji maji ya kunywa, mmoja usiokula sio ulioumbwa kwa mavumbi ya dunia. Lakini uko, ni halisi sana; na unaweza kuhisi na kupeana mikono, na kupenda tu, na kila kitu ni kikamilifu. Na huo mwili unangojea kule ng;ambo ni sehemu ya huo iko mitatu.

Unaanza uzima wa milele hapa madhabahuri. Hapa ndipo unaanza umilele. Oh unaanza uzima wa milele hapahapa. Hapa sasa umezaliwa mara ya pili kama mwana wa Mungu. Na hapo sasa unapokufa unaanza………..kifo kinapokukuta katika mwili huu na moyo unaacha kudunda, na gurudumu la uhai linaposimama, ile sehemu ndogo kivuli ambayo ilikuwa kivuli cha kivuli, katika sekunde moja inakuwa kivuli ya kivuli, halafu baadaye inakuwa kivuli, na baadaye inakuwa kamchirizi kadogo halafu inakuwa kijito kidogo, halafu inafuatia inakuwa mto, a baadaye inakuwa bahari, na baada ya muda umesimama uweponi pa wapendwa wako uliowapenda kule ng'ambo, ukiwa umevalia nguo za mwili wa kimbinguni, mnafahamiana mmoja kwa mwingine, mnapendana mmoja kwa mwingine. Umegeuka na kuwa kijana mvulana na kijana mwanamke tena. Hiyo ni sahihi kabisa. Inasubiri pale mpaka wakati wa kuja kwa Bwana Yesu.

Sasa, kumbuka, kuna mwili wa kimbinguni na siyo wa utukufu, ni mwili wa kimbinguni.

Na sikumoja mwili ule wa kimbinguni utaondoka mbinguni pamoja na Yesu.

"Kwa maana nasema hili kwenu, 1Wathesalonike 4:13-18 miili hii ya mbinguni inakuja duniani kuchukua miili ya duniani iliyotukuzwa. "Na sisi tulio hai tutakaosalia tutabadilishwa kwa kufumba na kufumbua tutanyakuliwa pamoja nao kumlaki Bwana hewani"



Ndugu Branham alituambia ushuhuda wake ufuatao wa mwaka 1960.

Jumapili iliyopita niliamka mapema. Hiyo ilikuwa Jumamosi; ono hili. Daima nimefadhaika. Daima nimefikiri juu ya kufa. Mimi, nikiwa na umri wa miaka hamsini, wakati wangu si….sidhani ilikuwa muda mrefu sana. Sijui nitakavyokuwa katika mwili huu wa Kiungu – mwili wa kimbinguni. Je! Itakuwa kwamba ningewaona marafiki wangu wapendwa na kuona ukungu mdogo ukipita na kusema, "huyo hapo Ndugu Neville anaenda" ama hangaliweza kusema, "Aloo. Ndugu Branham"? Na wakati Yesu atakapokuja, ndipo ningekuwa mtu tena. Nilifikiria jambo hilo mara kwa mara.

Nilikuwa ninaota ……" Nami nikaamka. Nikawaza, "ninaota sana. Sijui kwa nini" Nami nikaangalia chini naye alikuwa amelala karibu nami. Basi nikainuka kwenye mto wangu, kama vile wengi wenu enyi watu mmefanya. Nikaweka kichwa changu kwenye ubao wa kichwani wa kitanda na kuweka mikono yangu nyuma yangu. Nami nilikuwa nimelala pale namna hii kisha nikasema, "vema, sijui tu jinsi itakavyokuwa, ng'ambo ya pili. Mimi tayari nina umri wa miaka hamsini, nami sijafanya kitu bado. Laiti ningalifanya kitu fulani tu kumsaidia Bwana kwa maana najua sitakuwa anayepatikana na mauti Nusu ya wakati wangu imepita, lakini ama zaidi ya nusu. Kama nikiishi kuwa na umri wa watu wangu, hata hivyo nusu ya wakati wangu imekwisha. Nami nikaangalia kila mahali na nilikuwa nimelala pale nikijaribu kuamka. Ilikuwa kama saa 1:00 nikasema, "Naamini nitashuka niende kanisani asubuhi ya leo. Kama nikipwelewa na sauti, ningetaka kumsikia Ndugu neville akihubiri"

Kwa hiyo, nikasema, "U macho, Mpenzi?" Naye alikuwa amelala fofofo.

Basi sitaki mlikose jambo hili. Limenibadilisha. Siwezi kuwa Ndugu Branham yeye yule niliyekuwa.

Ndipo nikaangalia, nami nikasikia kitu kilichoendelea kusema "umeanza tu piga vita endelea kukaza mwendo"

Nikakitikisa kichwa changu kidogo kisha nikawaza, "vema, labda ninawazia tu namna hii mwajua, mtu anaweza kupata mawazo" nami nikasema, "labda niliwazia hayo tu hayo"

Ikasema, "piga vita! Endelea kusonga mbele! Endelea kusonga mbele!"

Nami nikasema, "Labda mimi nilisema jambo hilo"

Nami nikaweka midomo yangu kwenye meno yangu, na kuweka mkono wangu juu ya kichwa changu, na hiyo hapo ikaje tena. Kasema, "Endelea tu kukaza mwendo. Laiti ungalijua kilichokuwa kwenye mwisho wa safari".

Nami nikasikia kitu kikisema, "Ungetaka kuangalia ng'ambo ya pazia?"

Nikasema, Lingenisaidia sana" Nami nikatazama, na katika dakika moja, ni ………kupumua mara moja, nilikuwa nimefika mahali padogo ambapo paliinama. Nikatazama nyuma, nami huyo pale nimelala kitandani. Ndipo nikasema, "hii ni jambo la ajabu".

Sasa, nisingewataka ninyi mrudie jambo hili. Hili ni mbele ya kanisa langu, ama kondoo wangu ninaowachunga. Ama ilikuwa kwamba nilikuwa katika mwili ama nje yake, ama ilikuwa kuhamishwa…..Haikuwa kama ono lolote nililopata kuona. Ningeangalia pale, na ningeliangalia hapa. Na nilipofika mahali pale padogo, sijawahi kuona watu wengi hivi wanaokuja mbio, wakipiga kelele, "loo, ndugu yetu wa thamani" nami nikaangalia na vijana wanawake, labda kwenye umri usiozidi sana miaka ishirini (kumi na minane hadi ishirini) walikuwa wananikumbatia na kupiga kelele, "Ndugu yetu wa thamani"

Huyu hapa kijana anakuja katika uangavu wa utu uzima na macho yao yanang'ara na kuonekana kama nyota katika usiku wenye giza, meno yao meupe kama lulu, nao walikuwa wakipiga kelele na kunishika (kukumbatia) na kupiga kelele, "Loo, ndugu yetu wa thamani" Nami nikasimama na kutazama, nami nilikuwa kijana. Nikaangalia nyuma kwenye mwili wangu mzee umelala pale na mikono yangu nyuma ya kichwa changu basi nikasema, "sielewi jambo hili" na hawa vijana wanawake wakinikumbatia kwa mikono yao.

Naam, natambua ya kwamba huu ni umati uliochanganyikana, nami nasema hili kwa utamu na uzuri wa Roho. wanaume hawawezi kuwakumbatia wanawake bila ya msisimko wa kibinadamu. Lakini haukuwepo hapakuwepo na jana wala kesho. Wao hawakuchoka. Wao walikuwa………..sijapata kuona wanawake warembo jinsi hiyo maishani mwangu mwote, Nywele zao zilikuwa zimefika hata kiunoni, rinda ndefu zilizofika miguuni, nao walikuwa wakinikumbatia tu. Hakikua kikumbatio kama kile ambacho hata dada yangu anayeketi pale angenikumbatia. Hawakuwa wakinibusu, nami sikuwa nikiwabusu. Kilikuwa kitu ambacho sina msamiati; sina maneno ya kusema. Ukamilifu halingeligusa. Kipeo hata halingaliligusa popote. Kilikuwa kitu ambacho kamwe sija……Itakubidi tu kuwa kule.

Nami nikatazama huku na huko, nao walikuwa wakija kwa maelfu. Nami nikasema, 'sifahamu jambo hili" Nikasema, "mbona wao……"Na huyu hapa Hope anakuja – huyo alikuwa mke wangu wa kwanza. Yeye alikimbia na - hakusema kamwe, "Mume wangu. "Alisema, "Ndugu yangu mpendwa" Na wakati aliponikumbatia, palikuwepo na mwanamke mwingine amesimama hapo aliyekuwa amekwisha nikumbatia ndipo Hope akamkumbatia mwanamke huyu na kila mmoja



Nami nikafikiri, Loo, hili halina budi kuwa ni jambo tofauti, haiwezekani. Kuna kitu……..Loo, singalitaka kamwe kurudi kwenye maskini mzoga ule tena?" Nikaangalia kila mahali pale na kuwaza, "Ni nini hii?" nami nikaangalia kwa makini sana, ni – nikasema, "Si – siwezi kufahamu jambo hili" Bali Hope alionekana kama………loo mgeni wa heshima. Hakuwa tofauti lakini kama tu mgeni waheshima.

Ndipo nikasikia sauti wakati huo iliyonena nami iliyokuwa chumbani, kasema, "Hii ndiyo uliyohubiri kuwa ni Roho Mtakatifu. Huu ndio upendo mkamilifu. Na hakuna kinachoweza kuingia humu bila huo"

Nimeazimia sana kuliko wakati wowote maishani mwangu ya kwamba inahitaji upendo mkamilifu kuingia mle. Hapakuwa na wivu. Hakukueko na uchovu. Hakukuweko na mauti. Magonjwa hayangeweza kuingia mle. Kupatikana na mauti hakungeweza kukufanya mzee, nao hawangeweza kulia. Ilikuwa tu furaha moja – "Loo, ndugu yangu mpendwa"

Nao wakanichukua na kuniweka juu ya mahali pamoja pa juu. Nami nikawaza, "Mimi sioti ndoto. Ninaangalia kule nyuma kwenye mwili wangu uliolala kule chini kitandani" Nao wakaniweka mimi pale nami nikasema, "loo, hainipasi kuketi hapa juu."

Na hapa wakaja wanawake na wanaume kutoka pande zote mbili katika tu ukamilifu wa ujana, wanapiga kelele na mwanamke mmoja alikuwa amesimama pale naye anapiga kelele, "loo, ndugu yangu mpendwa. Loo, tunafurahi kukuona hapa"

Nikasema, "mimi sifahamu jambo hili"

Ndipo sauti hiyo iliyokuwa ikinena nami kutoka juu yangu ikasema, "unajua imeandikwa katika Biblia ya kwamba manabii walikusanywa pamoja na watu wao"

Nami nikasema, "Naam, nakumbuka jambo hilo katika maandiko"

Kasema, "Lakini, huu ni wakati utakapokusanyika pamoja na watu wako"

Nikasema, "lakini mimi…….kuna mamilioni. Hakuna Wabranham wengi namna hiyo"

Na sauti hiyo ikasema, hao si Wabranham; hao ni wale uliowavuta. Hao ndio ambao uliowaongoza kwa Bwana" Kisha kasema. "baadhi ya hao wanawake pale unaofikiri ni warembo sana walikuwa zaidi ya miaka tisini ulipowaongoza kwa Bwana. Si ajabu wao wanapiga kelele, ndugu yetu mpendwa"

Nao wakapiga kelele mara moja, kasema, “kama haungalikwenda, hatungalikuwa hapa.”

Nikaangalia kila mahali nikawaza, “Vema, sijafahamu” Nikasema, “Loo, yuko wapi Yesu? Nataka kumwona vibaya sana”

Wao wakasema, “Naam, yuko juu kidogo tu moja kwa moja upande ule” kasema, siku moja yeye atakuja kwako” Mnaona? Kasema, “wewe ulitumwa kuwa kiongozi na Mungu atakuja na atakapokuja Yeye atakuhukumu kulingana na yale uliyowafundisha, kwanza; kama wataingia ama hawataingia tutaingia kulingana na mafundisho yako”

Nikasema “Loo ninafurahi sana je, Paulo – yeye itambidi kusimama namna hii? Itambidi Petro kusimama namna hii?

“Naam”

Nikasema, Basi nilihubiri kila neno walilohubiri. Sikuhitilafiana kutoka upande mmoja kwenda mwingine. Walipobatiza katika jina la yesu Kristo, nilibatiza pia walipofundisha ubatizo wa Roho Mtakatifu, nilifundisha pia kila walichofundisha, nilifundisha pia”

Ndipo hao watu wakapiga kelele wakasema, “tunajua jambo hilo nasi tunajua tunarudi pamoja nawe siku moja duniani” kasema, “Yesu atakuja, nawe utahukumiwa kulingana na neno ulilotuhubiria sisi. Halafu kama ukikubalika wakati huo, ambapo utakubalika” kisha kasema “basi wewe utatukabidhi kwake kama tunu yako ya huduma yako” kasema, “utatuongoza kwake na sote pamoja tutarudi duniani tukaishi milele”

Nikasema, “inanibidi kurudi kule sasa?”

“Ndiyo, bali endelea kukaza mwendo”

Nikaangalia, nami ningeweza kuwaona hao watu; umbali nilioweza kuona, wangali wanakuja, wakitaka kunikumbatia, wakipiga kelele, “ndugu yetu mpendwa”

Mara sauti ikasema, “Kila ulichowahi kupenda, na kila kilichowahi kukupenda, Mungu amekupa wewe hapa” Nami nikaangalia na huyu hapa mbwa wangu wa zamani anakuja.

Huyu hapa farasi wangu anakuja na kukilaza kichwa chake juu ya bega langu na kulia. Kasema, “kila ulichowahi kupenda na kila kilichowahi kukupenda, Mungu amevikabidhi mikononi mwako kupitia kwa huduma yako”



Nami nikajisikia nikitoka mahali hapa pazuri. Nilipo, nikaangali kila mahali nikasema, “U macho, Mpenzi? Alikuwa angalia analala. Nami nikawaza, “Ee Mungu, lo nisaidie ee Mungu, Usiniache kamwe nipatane kwa neno moja. Nijalie nidumu sawasawa katika Neno hilo na kulihubiri. Sijali nini kinachokuja ama kinachokwenda, kile mtu yeyote afanyacho, ni Sauli wangapi ama wana wa Kishi watainuka ni wangapi hawa, wale na wengineo, nijalie mimi, bwana, kukaza mwenendo nipafikie mahali pale.

Hofu yote ya mauti…….nasema jambo hili huku Biblia yangu ikiwa mbele zangu asubuhi ya leo. Nina kijana mdogo pale, mwenye umri wa miaka minne, wa kulea. Nina msichana mwenye umri wa miaka tisa na msichana tineja ambao ninashukuru kwa ajili yao, ambao wameishika njia ya Bwana. Mungu na anijalie niishi nipate kuwalea katika maonyo ya Mungu. Juu ya hayo, inaonekana kama kwamba ulimwengu mzima unanipigia kelele. Wanawake na Wanaume wenye umri wa miaka tisini na wa namna zote, “kama usingelienda, tusingeweza kufika hapa na Mungu, nijalie niendelee kupigana vita lakini kama ikifikia kufa, mimi si nini zaidi……..Inakuwa ni furaha, ingekuwa furaha kuingia kutoka upotovu huu na aibu.

Kama ningalifanya kule ng’ambo maili bilioni mia moja kwenda juu, kipande cha mraba na hicho ni upendo mkamilifu. Kila hatua upande huu, inasonga, hata tunapofikia mahali tulipo sasa. Ingekuwa tu ni kivuli cha upotovu. Hivyo kitu fulani kidogo tunachoweza kuhisi na kusikia ya kwamba kuna kitu fulani mahali fulani; hatujui ni nini. Lolo. Rafiki zangu wapendwa, wapendwa wangu, wapenzi wangu wa Injili, watoto wangu niliomzalia Mungu, nisikilizeni mimi, mchungaji wenu. Ninyi………..Laiti kungalikuwa na njia ningaliweza kuwaelezea ninyi. Hakuna maneno. Nisingeyapata. Hayako popote. Bali ng’ambo tu ya huku kupumua kwa mwisho ni jambo lenye utukufu sana mlilowahi…….Hamna njia ya kulielezea. Hamna njia; siwezi tu kufanya hivyo. Bali chochote ufanyacho, rafiki, weka kando kila kitu hata utakapopata upendo mkamilifu. Fikia mahali ambapo unaweza kumpenda kila mtu, kila adui, chochote kile. Huko kuzuru kwangu kumoja kule kumenifanya mtu tofauti. Siwezi kamwe, kamwe, kamwe kuwa ndugu Branham yeye yule niliyekuwa.

Huu mwili wakufa unavaa kutokufa. Mwili huu wa dunia unachukuwa mwili wa mbinguni unaona ninachomaanisha? Kuna mwili wa asili ambao ni wa dhambi (Warumi 6:12); Lakini katika kule kuumbwa kwake ni kama tu mwili mwingine ambayo tutachukua. Na ninamshukuru sana Mungu kwamba ninaweza kusema kama mchungaji wenu na ndugu yenu, niliwaona wale watu, Hivyo nisaidieni katika miili ile niliwashika na mikono yangu hiyo ni sawa.

Angalia, uone, mwangalie Musa, Eliya, baada ya kuwa Musa alikuwa amekufa na Eliya amechukuliwa juu mbinguni, walisimama pale katika mlima wa

kugeuzwa wakiwa na hisia zake za kunena, kusikia, kuelewa na wanazungumza na Yesu kabla ya kule kusulubiwa (Matayo 17:1-8).

Sasa, ni mwili wa aina gani alikuwa nao? Mwangalie Samweli. Baada ya kuwa amekuja kama miaka miwili, aliitwa kule pangoni usiku ule na yule mchawi/mganga wa Endori na akazungumza na Sauli katika lugha, aliyoisikia sauti, naye alijibu, na alijua mambo kimbele yale ambayo yangetokea; bado roho yake haijabadilika yeye alikuwa ni nabii (1Samwel 28:7-19).

Hii ni Roho inayokufa inayokaa katika mwili unaokufa; lakini sasa huwezi ukawa katika miili miwili kwa wakati mmoja, lakini kilichotokea, ni kuzaliwa kiroho kumekuja kwako (Yohana Mt 3:1-8; 1Petr 1:22-23). Na wakati huku kuzaliwa kiroho kunakuwa ndani ya moyo wako, kwa Mungu, kuna mwili, mwili wa kimbinguni unaokuwa, kupokea ile roho (2 Petr 3:18). Na wakati uhai unapoondoka katika mwili, unaenda kwa mwili ule. Kama tu vile mwili unapodhihirishwa duniani Roho inaingia ndani, na wakati Roho inapoondoka katika mwili, upo mwili ambao unangojea. "kwa maana tunajua kwamba mwili huu wa dunia unapokaribia,tunalo kao lingine tayari linatungojea" unaona? Hiyo ndiyo hasa, miili ya kiroho ya watu.

Sasa, huo ni mwili wa kimbinguni, ambao tunapokufa hatuwi kitu cha kuwazia; tunakuwa katika mwili kama kila mmoja wetu atakufa, kama bomu la atomiki litatulipua dakika hii, katika dakika tano kutoka sasa tutakuwa tunapeana mikono mmoja kwa mwingine na kukumbatiana shingoni na kupiga makelele, na kufurahi na kumtukuza Mungu, ndiyo, Bwana.

Na imenisaidia mimi, kwa sababu nilikuwa na wazo kuwa mtu akifa, ni nafsi yao tu iliyotoka. Lakini aliponinukulia haya, "kama maskani yetu iliyo ya dunia ikiharibiwa, tayari tunalo lingine (2 Kor 5:1). Unaona? Na inabidi kila kitu kiwe katika utatu ili kikamilike unaona? Na kuna mwili mmoja hapa, na ule mwili pale ambao ni wa kimbinguni, na halafu uko mwili wa utukufu katika ufufuko. Unaona hilo linafanya ukamilifu unaona? Kwa hiyo siyo jambo la kuwazia; sio wazo; sio Roho ni mtu mume na mwanamke kama ulivyohasa hiyo ni sawa.

Na miaka iliyopita niliona maeneo ya waliopotea na walikuwepo pale. Ninakuambia rafiki. Kama mtu mzima, hebu nikushawishi hili, kupita nchi yote asubuhi hii, usipende kuliona hilo eneo hakuna njia hata kidogo niwezayo…………Hata ningekuwa mchoraji na brushi nisingeweza kuichora licha yake kama mhudumu, nisingeweza kukuelezea wewe zungumzia kuzimu kuwa ni mahali pa motoni, ni mara milioni ya hapo ubaya wake, hiyo huzuni inayoenda na hilo.

Na mbinguni………au hapa mahali iwavyo vyote, sijui nipaiteje. Alipazungumzia kama "Roho zilizochini ya madhabahu" lakini nilipopaona,



kamwe siwezi kuelezea; hakuna njia ya kupaelezea palivyo pakuu. Sasa, inabidi tu uchukue Neno langu mimi ni mtu tu unaona? Lakini haya maono ambayo mara zote yamekuwa kweli kama nilivyowaambia, na mnajua kila moja limekuwa ni kweli; hilo ni kweli pia chochote ufanyacho, kama utakosa kitu kingine chochote (afya, nguvu, macho yasione, chochote kiwacho), usikose hilo. Hakuna chakulinganishwa na hilo. Hakuna maneno katika lugha ya kiingereza ambayo ninaijua ambayo inaweza kuelezea hilo. Ukisema ni "kamilifu" ni zaidi ya hiyo; "kipeo cha uzuri" ni zaidi ya hapo; "tukufu mno ya kifahari"…..Hakuna maneno nijuayo yawezayo kuelezea hilo, kwa sababu iko hivyo……Na halafu, kufikiria, bado huo sio mwisho wake bado.

"Lakini kama ilivyoandikwa, mambo ambayo jicho halikuyaona wala sikio halikuyasikia wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu. Mambo ambayo Mungu amewaandalia wampendao.

**Nukuu za kiingereza:**

"uzima" (57-0602), Aya 22-24
"Isikie sauti yake" 58-1005m, Aya 11-14
"maswali na majibu" (61-0112), swali na 117 uk. 561, Aya 122
"Kusikia, kutambua, na kulitendea kazi Neno" (kitabu 13 na 7), Aya 135-139
"wana wa Mungu walioadhimishwa" kufanywa wana sehemu ya 2 Aya 65-71
"Mfalme aliyekataliwa (kitabu 2 na 23) uk 19-23, Aya 54-63
Mhuri wa tano" kitabu cha mihuri uk 387, Aya 161-162
"maswali na majibu" 64-0830E, Swali no 381, uk 1156, Aya 35 mahali pekee Mungu alipopachagua pakuabudia (kitabu 7 na 4) Aya 22-24

---

*Jiwe la kiroho la kujengea na 100 kutoka Neno lililofunuliwa la saa hii. Iliyokusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69-D– 75328 Schomberg Germany Simu (+49) 7235 - 7613. Fax (+49) 7235 3306.*

---

*Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia, zile mbegu zitaingizwa magazetini na vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu ya Mungu iliyochaguliwa kimbele imesikia hilo (Ndg. Branham katika mwenendo na mafundisho uk 724)*

*Kwa nakala zaidi za kiingereza na kiswahili. Andika kwa: Charles E. Y. Kanju*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*